# Vunja UKIMYA Ondoa VIKWAZO!

## Unawezaje kufanya Elimu kuwa Salama kwa Wasichana?

**Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia**

**Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Unyanyasaji wa Kijinsia Mwaka 2016**

**Mwongozo wa Shughuli za Kampeni**

GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum • Fostering Activism

## *Vunja Ukimya, Ondoa Vikwazo! Unawezaje Kufanya Elimu Kuwa Salama kwa Wasichana?*

Zaidi ya miaka 25 wanaharakati na watendaji mbalimbali duniani kote wametumia Siku 16 za kipindi cha Harakati kuainisha Ukatili wa Kijinsia kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Mwaka huu tutajikita katika kufanya elimu kuwa salama kwa wote, hasa kwa wasichana na wanawake vijana.

Kwa kutumia aina mbalimbali za shughuli kwa Kushirikiana na Mashirika na wadau tutaweza kuvunja ukimya kwenye jamii zetu na shuleni kwa kuweka wazi vikwazo vya wanawake na wasichana katika upatikanaji wa elimu na masuala ambayo yanasababisha maeneo ya utoaji elimu kutokuwa salama. Baadhi ya masuala yaliyoainishwa ni pamoja na; vikwazo vya uandikishaji wasichana na kuhakikisha wanaendelea na masomo kwa mfano: ndoa za utotoni, athari za kiusalama njiani wakati wa kwenda shuleni kama vile unyanyasaji wa kijinsia, usalama ndani ya shule kwa mfano, kutofautisha miundombinu ya vyoo, na vikwazo katika mfumo wa elimu kwa mfano, mitaala ya shule inayohamasisha ubaguzi wa wanawake na wasichana.

Mwongozo huu wa shughuli za Kampeni ni mapendekezo ya hatua na shughuli zinazoweza kufanyika ili kuifanya kampeni yako kuwa yenye ubunifu na jumuishi kwa kadiri iwezekanavyo. Unaweza kuongeza maelezo mengine katika shughuli utakazo chagua kuzifanya zinazo endana na mazingira yako.Tafadhali tujulishe jinsi shughuli hizi zitakavyo fanyika tuna shauku kusikia kutoka kwenu!

### Maandalizi kwa Ajili ya Kampeni Yako

1. **Hatua ya 1:** Soma nukuu ya Kampeni inayopatikana katika kitini ili uweze kuelewa vizuri kuhusu masuala yanayo shughulikiwa katika kampeni.
2. **Hatua ya 2:** Soma na ukamilishe Karatasi kazi ya Kampeni pia katika kitini hiki na uamue juu ya suala moja au mawili ambayo ni vikwazo vikubwa zaidi katika elimu kwenye jamii yako.
3. **Hatua ya 3:** Fanya mkutano na wafanyakazi wenzako ili kupanga na kuanisha mambo muhimu katika kampeni yako. Katika mkutano huo unaweza kuchagua kutoka kwenye baadhi ya shughuli zifuatazo.
4. **Hatua ya 4:** Kumbuka kuwa na furaha wakati unavunja ukimya unaohusiana na vikwazo vya elimu kwa wasichana

## *Shughuli Zinazopendekezwa Katika Kampeni*

### Vunja Ukimya na Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari ni nyenzo yenye nguvu katika kubadili mitazamo, imani na matendo katika jamii zetu. Ikiwa kwa makusudi tutaweza kushirikisha vyombo vya habari wakati wa Siku 16 za kampeni basi tunaweza kutumia hii nyenzo yenye nguvu na ushawishi mkubwa kuvunja ukimya na kuainisha vikwazo ndani ya nyumba zetu, jamii na shuleni katika uandikishaji wa wasichana na kuhakikisha wanamaliza shule. Matumizi ya kimkakati ya vyombo vya habari haitahusu tu kuonyesha shughuli zetu na vikwazo vyetu juu ya elimu kwa wasichana lakini pia inaweza kuwa kichocheo kitakacho leta mabadiliko mapana. Yafuatayo hapo chini ni mapendekezo, mawazo kwa ajili ya uanaharakati na vyombo vya habari.

- **Mkutano na Vyombo vya Habari:** kwa kawaida shughuli hii hupangwa kwaajili ya kutangaza habari muhimu kwa idadi kubwa ya waandishi wa habari. Karibisha vyombo mbalimbali vya habari katika mkutano wako wa waandishi wa habari na ainisha vikwazo vya elimu kwa wasichana katika jamii yako ukitoa mapendekezo yako ili kushughulikia swala hili. Hakikisha

kwamba tangazo lako lina ushawishi mkubwa kwa vyombo vya habari ili uweze kuleta mvuto kwa vyombo vya habari katika suala hilo.

- **Mazungumzo na Waandishi wa Habari:** hii sio shughuli rasmi zaidi ya mkutano wa vyombo vya habari na unaweza kutumia fursa hii kuwajulisha waandishi wa habari juu ya shughuli zako ulizopanga kwa ajili ya kampeni vile vile shughuli za mashirika mengine katika mji wako na katika Pembe ya Afrika, Mashariki na Kusini mwa Afrika.

- **Matangazo ya Radio na Runinga:** Unaweza kuyatumia kuleta mvuto kwa tukio lako lakini pia kuainisha masuala yanayoshughulikiwa na Kauli mbiu ya Kampeni. Matangazo ya runinga yanaweza kuwa ghali kuyaonyesha lakini unaweza kumtumia mtu anaeheshimiwa sana na kuomba vyombo vya habari kutoa muda wa vipindi vitakavyoonyshwa bila malipo yaani mradi usiotengeneza faida (kwa njia hiyo ninyi wote wawili mtafaidika)

- **Machapisho / Makala katika Magazeti:** Kwa kutumia maudhui ya Kauli mbiu ya Kampeni kama mwongozo unaweza kushirikisha watoto wa shule, walimu na viongozi wa shule katika kuandika makala, Maoni ya Wahariri (Op Eds), au barua kwa mhariri. Hakikisha unaifanya habari hii kuwa na uzito mkubwa ili iweze kuleta ushawushi mkubwa kwenye vyombo vya habari ili iweze kuchapishwa na kusaidia kuvunja ukimya kuhusu vikwazo vya elimu kwa wasichana

- **Kampeni ya Ujumbe Mfupi wa Maneno:** Kampeni ya ujumbe mfupi wa maneno ni moja ya njia bora tunayoweza kuitumia kutangaza mawazo yetu kwa watu wengi walio sehemu mbalimbali. Idadi kubwa ya watu wanatumia simu za mkononi katika kanda yetu na wengi zaidi wanawasiliana. Tunaweza kutumia fursa hii kuvunja ukimya na kuongeza uelewa kuhusu vikwazo vya elimu kwa wasichana

- **Kampeni Katika Mitandao ya Jamii:** Majukwaa ya mitandao ya kijamii yanazidi kuwa maarufu katika kusambaza habari na kuhamasisha jamii kuhusu suala fulani. Tumia majukwaa yako ya mitandao ya kijamii kuhamasisha na kujenga uelewa kuhusu vikwazo vya elimu kwa wasichana katika jamii yako, hakikisha unashirikisha kurasa nyingine za mitandao ya kijamii zinazotembelewa sana. Kampeni ya mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia itakuwa imeingizwa kwenye Kampeni ya mitandao ya kijamii kimataifa ikiratibiwa na Kituo cha Uongozi wa Wanawake Duniani. Halikadhalika tutatoa taarifa mpya kila siku kwenye kurasa yetu juu ya shughuli zako. Tafadhali hakikisha unatutumia taarifa za shughuli zako katika **info@preventgbvafrica.org** ili tuweze kushirikisha wadau wengine katika kanda. Fuatilia zaidi katika @GBVNet na Facebook (Mtandao wa Kuzuia Ukatili Kijinsia).

- **Redio za Jamii:** Jamii mbalimbali zinazoishi vijijini zina sikiliza redio za jamii. Mara nyingi redio hizi husikika siku ya soko na hupatikana katika vituo vya biashara. Wadau wenye Redio za jamii wazitumie katika siku hizo za harakati ili kuvunja ukimya kuhusu vikwazo vya upatikanaji wa elimu kwa wasichana. Kwa mfano, unaweza kufanya mahojiano ambayo yataainisha vikwazo vya upatikanaji wa elimu salama kwa wasichana.

## Ushiriki wa Jamii Katika Shughuli

**Mazungumzo Mafupi:** Tumia bango na muongozo wa maswali ya majadiliano ya bango kwenye kikundi kidogo. Tumia ili kupanda mbegu ya wazo na kuhimiza liweze kukua. Shawishi watu katika jamii kwa kufanya mazungumzo papo kwa papo pamoja nao. Ushiriki katika mazungumzo mafupi ni njia muhimu ya kufanya watu wazungumze. Unaweza kufanya mazungumzo haya na majirani, marafiki, ndugu, wageni katika foleni, sokoni katika teksi, na mahali popote. Mazungumzo mafupi huchochea kufanya majadiliano. Watu unaofanya nao mazungumzo sio lazima wakubaliane na hoja yako – usijisikie vibaya kuwashawishi kuhusiana na mtazamo wako, kuanzisha mada mpya inaweza kufungua njia mpya ya kufikiri na kuleta mabadiliko.Unaweza kutembea kwa haraka hadi kwenye kikundi kidogo cha watu, tabasamu, salimiana nao, anzisha mazungumzo ili kujadili mada moja au mbili katika mwongozo wa bango la majadiliano, funga mazungumzo na kuwaachia mawazo machache ambayo ungependa waendelee kutafakari. Fanya mjadala chanya na yenye kufurahisha! (Unaweza kufanya vizuri zaidi kama utafanya mazoezi na wenzako kabla ya kuanza kwa kampeni)

**Maonyesho ya Wazi na Maigizo:** Tumia vikundi vya maigizo vya kijamii kushirikisha na kuelimisha jamii juu ya kauli mbiu. Jamii mbalimbali wana tamaduni ya kusimulia hadithi. Watu wanapenda kujifunza kuhusu wao wenyewe na maisha yao kwa njia ya hadithi. Matumizi ya maigizo yanatumia utamaduni ili kuonyesha yanayotokea katika jamii. Lengo la michezo ya kuigiza ni kuelimisha na kuhamasisha majadiliano. Ili kupata matokeo mazuri zaidi ya maigizo yako tumia mtu wa kuongoza majadiliano kila baada ya kipengele cha igizo kuisha ili kufanya maigizo yawe shirikishi. Hakikisha maswali ya mjadala yanaulizwa katika mfumo shirikishi, kutia msisimko, na kuhamasisha wanajamii kufikiria na kufanya mambo tofauti. Muziki na maigizo yanaweza kushirikisha watoto wa shule kwa kushirikiana na vikundi vya kijamii vya maigizo.

**Midahalo Katika Jamii:** Midahalo ya jamii ni njia kuu inayowezesha watu kujumuika pamoja na kujifunza na kushirikisahana masuala ya kijamii. Unaweza kuendesha mdahalo mkubwa wa jamii mchana, wakati wa mdahalo; waombe wanajamii kujadili masuala mbalimbali yanayoathiri elimu ya wasichana katika jamii yako. Baada ya mdahalo, fanya mkutano mdogo na watu maarufu / viongozi / watu wenye ushawishi mkubwa katika jamii hiyo (watu 15-30) (unatakiwa kuwa makini kuhakikisha kwamba viongozi hawa watashiriki kwenye  mdahalo mkubwa) Katika mkutano mdogo viongozi hawa wanapaswa kutoa azimio moja kubwa (liandike na uwaombe waweke sahihi) kuhusu jinsi watakavyoboresha elimu ya wasichana katika jamii yako

**Kuwatumia Watu Maarufu:** Jamii mbalimbali kuna watu ambao maoni yao huheshimiwa. Kwa kutumia watu wenye ushawishi mkubwa inaweza kukusaidia katika kushawishi mitazamo. Tambua baadhi ya watu wenye ushawishi mkubwa sana katika jamii yako (waalimu wakuu wa shule, Viongozi wa kisiasa, Viongozi wa dini, Viongozi wa Kimila, Wazazi,Watu Maarufu nk) warekodi wakizungumza kuhusu elimu kwa wasichana, ujumbe wa kila mtu uwe mfupi usizidi dakika 3-5. Baada ya kurekodi video endesha tamasha kubwa la jamii baadaye  wakati wa jioni waonyeshe  video hiyo jamii nzima. Kwa kawaida, inaleta msisimko kwa sababu jamii wanawaona watu wanaoishi nao katika jamii moja wanatoa mawazo muhimu sana kwa kuangalia video ile. Shughuli hii inahitaji asasi yako iwe na uwezo, ujuzi na vifaa vya kurekodi na kuonyesha video.

**Michezo na Mashindano:** Andaa michezo na mashindano kwa watoto na watu wazima. Kwa siku yenye hamasa zaidi changanya aina mbalimbali za michezo – mchezo wa bao, mpira wa pete, mpira wa miguu, mbio za baiskeli, mchezo wa mieleka n.k tumia fursa hii wakati kila mtu amepumzika na kua na hisia chanya kujadili na kuanisha vikwazo vya elimu kwa wasichana katika jamii yako. Kuchangamsha zaidi unaweza kuwaandaa wasichana wacheze michezo inayoonekana kuwa 'ya wanaume' na kinyume chake. Wazo ni kuvunja unyanyasaji wa kijinsia lakini pia kuhamasisha wasichana wasizimishe ndoto zao kwa sababu ya jinsia yao

**Matembezi ya Hisani:** Pamoja na wafanyakazi wa shirika lako, wadau kutoka mashirika na wanaharakati wa jamii andaa na endesha matembezi ya hisani katika jamii yako na kutumia fursa hiyo kuongeza uelewa juu ya vikwazo vya elimu kwa wasichana. Hakikisha unalenga maeneo katika jamii ambayo yana idadi kubwa ya watu. Unaweza kuamua kuzunguka na bendi au matangazo ya wazi au tumia ngongoti kuvutia watu. Gawanya majukumu kimkakati ili ndani ya timu wawepo na wafanyakazi wenzako wenye machapisho kama vile vipeperushi ambavyo vina taarifa kuhusu vikwazo katika jamii yako. Wahusika katika timu yako wajigawe katika eneo husika ili kusambaza vipeperushi hivyo na kufanya majadiliano juu ya masuala husika na makundi madogo madogo ya watu.

## Uanaharakati Shuleni

**Midahalo:** Simamia majadiliano shuleni juu ya vikwazo wanavyokumbana navyo wasichana katika upatikanaji wa taarifa katika mazingira mbalimbali (nyumbani, shuleni na katika jamii) unaweza kuwa na majadiliano tofauti kwa ajili ya watoto, walimu, na wazazi katika siku tofauti. Tumia zoezi hili kutambua wahusika wakuu katika shule na jamii ambao wanashughulikia vikwazo vya elimu kwa wasichana

**Elimu Burudani:** Tumia fursa hii kuonyesha filamu, tumia muziki wa dansi na maigizo ili kuonyesha vikwazo vya elimu kwa msichana.